**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHURI YA MJI KASULU**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0759868746**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0767898247**

**Shule ya Sekondari Kigoma Grand**

**S.L.P 286 KASULU**

**Tarehe: 01/05/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ____________________________________**
**S.L.P ________________________________________________________**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIGOMA GRAND HALMASHAURI YA MJI WA KASULU MKOA WA KIGOMA MWAKA ……………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……………. na atasoma tahasusi ya __

Shule ya Sekondari KIGOMA GRAND ipo umbali wa Kilometa 7 Kaskazi kutoka stendi ya mabasi ya Mji wa Kasulu. Usafiri wa wa gari ndogo (mchomoko) na pikipiki/bajaji kutoka mjini Kasulu unapatikana katika kituo cha mabasi. Nauli ni Shilingi 2000/= kwa mchomoko na kwa pikipiki/bajaji ni Shilingi 3000/= tu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa amevaa sare za shule tarehe …………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. **Wasichana**: Sketi **02 dark blue** za linda box 2 kubwa, na linda nne ndogo lila upande. Sketi iwe ndefu hadi kwenye jicho la mguu

Rangi hiyo ni kwa ajili ya darasani tu.

**Wavulana**: Suruali ***02 dark blue*** zenye linda mbili kila upande na iwe na pindo kwa chini(yaani tan up). Hizi zinatumika kwa ajili ya shughuli za darasani tu.

ii. Mashati mawili 02 meupe mikono mirefu (*wasichana na wavulana*);

iii. Kwa wasichana wa **Kiislamu** wanapaswa kuja pia na Hijab (*kijuba*) rangi nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama kwa ajili ya kuvaa

iv. Kila mwanafunzi ajje na traki suti 01 yenye rangi ya dark blue,

v. Kwa wavulana pia aje na bukta 01 dark blue na raba nyeupe kwa ajili ya michezo.Kwa wasichana pia waje na raba nyeupe.

vi. Kila mwanafunzi aje na Viatu vyeusi pea 02 vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi pia kiwi nyeusi na brush ya viatu;

vii. Soksi jozi mbili **nyeupe** kwa wasichana zinazofika kwenye magoti na rangi nyeusi kwa wavulana tu.

viii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali usiwe wa utambi au inta;

ix. Sweta 1 la kijivu (*wavulana na wasichana*) ;

ix. **Nguo za kushindia** (*shamba dress*)

**WASICHANA:** Sketi 02 za rangi ya kaki mpauko zenye linda box 2 kubwa na ndogo 4 kila upande,sketi ziwe na urefu unaofika kwenye fundo la mguu.

**WAVULANA:**Suruali 02 za kaki mpauko zenye linda mbili na pindo kwa chini (TAN UP);

x. Tai 02 za rangi ya dark blue ndefu kiasi kwa wavulana tu;

xi. T- shirt 02 Rangi ya brown. Iwe na kola nyeusi na ufito mwesi mikononi (wavulana na wasichana);

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 counter books

ii. **Ream 2 (A4)** aina ya **Double A**;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;

| TAHASUSI | AINA YA VITABU |
|---|---|
| PHYSICS | 1. NECTA EXAMINATION REVIEW<br>2. Nelcon and Park<br>3. Chand I<br>4. Chand II<br>5. Rogerman chaster<br>6. Physics (TIE)<br>7. ABC physics volume I |
| CHEMISTRY | 1. NECTA EXAMINATION REVIEW<br>2. General chemistry (TIE)<br>3. Physical chemistry (TIE)<br>4. Inorganic chemistry(TIE)<br>5. Organic chemistry(TIE)<br>6. ABC chemistry<br>7. Chand I<br>8. Chand II<br>9. Advanced chemistry(Ramsden) |
| BIOLOGY | 1. Biology form five (TIE)<br>2. Biological science(BS)<br>3. NECTA EXAMINATION REVIEW |
| GEOGRAPHY | 1. Physical geography (TIE)<br>2. Practical geography (TIE)<br>3. Physical geography (Msabila)<br>4. Practical geography( Zist kamili)<br>5. Advanced current revision NECTA examination geography review |
| ADVANCED MATHEMATICS | 1. TIE,<br>2. PURE 1 $2 MATHEMATICS (BACKHOUSE<br>3. Understanding mathematics<br>4. Pure mathematics (Mayobya)<br>5. NECTA EXAMINATION REVIEW |
| BASIC APPLIED MATHEMATICS | 1. TIE<br>2. NECTA EXAMINATION REVIEW |
| GENERAL STUDIES | 1. General studies (TIE, )<br>2. General studies , (Mwandishi Bigirwamungu)<br>3. NECTA EXAMINATION REVIEW |

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Lab coat 01
vii. Kadi ya bima ya afya
viii. Gumboot kwa ajili ya kujikinga na tope;

ix. Aje na Godoro la futi 2.5.kwani hakuna magodoro ya kukodisha shuleni.

x. Mashuka rangi ya bluu bahari Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (nyeupe/bluu *bahari);*

x. Nguo za ndani za kutosha;

xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

xii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na dumu la lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa;

xiii. Kiti kimoja cha plastic aina ya **Cello**

xiv. Mopa 2 kwa mchepuo wa PCB tu

xv. Soft broom 1 na hard broom 1 kwa mchepuo wa CBG tu

xvi. Jembe na mpini wake kwa mchepuo wa PCM tu.

xvii. Aje na Bima ya afya kwa ajili ya matibabu.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote hiyo iingizwe kwenye Acount ya shule yenye **jina la KIGOMA GRAND SECONDARY SCHOOL CAPITATIONS FUND NMB 51410019372.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;


vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**SHULE YA SEKONDARI KIGOMA GRAND**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi ……………………………………. Dini /Dhehebu ……………….
2. Jina kamili la Baba ……………………………………………………………………….
3. Je Baba yuko hai au amefariki …………………………………………………………
4. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki ……………………………….
5. Jina kamili la Mama …………………………………………………….
6. Je mama yuko hai au amefariki ……………………………………………………
7. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki ………………………………………
8. Anuani ya Mzazi ……………………………S.L.P ……………………………………
9. Kazi aifanyayo Baba ………………………………………………………………………
9. Sehemu anayofanyia kazi ………………………………………………………………
11. Kazi aifanyayo Mama ………………………………………………………………………
12. Sehemu anakofanyia kazi ………………………………………………………………
13. Kama huishi na Mzazi wako taja jina la Mlezi wako …………………………………
14. Kazi aifanyayo………………………………………………………………………………
15. Sehemu anakofanyia kazi ………………………………………………………………
16. Anuani ya Mlezi ……………………………………… S.L.P ……………………………
17. Habari nyingine za familia ;

Jina la Kaka/Dada Umri kazi yake……………………………… Mahali anapofanyia kazi ……………………………………Kama ni mwanafinzi taja Shule.

(a) …………………… ………… ………………………………
(b) ……………………………………………………………………

18. Afya ya Mwanafunzi (Tafadhali eleza kama una ugonjwa wowote ambao una kukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu) Ni muhimu umfahamishe Daktari atakaye kupima ili naye aweze kujaza katika sehemu inayomuhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu ……………………………………………………………………………

19. Uthibitisho wa Mwanafunzi;

Nathibitisha kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.

Sahihi ……………………………………………………………………………………

Tarehe ……………………………………………………………………………………

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

(To be completed by a Medical officer in respect of all form Entrance)

Pupil's full name …………………………………………………………………………………

Age …………………………. (Year) …………………………. Sex ………………………

Stool examination ………………………………………………………………………………

Urinalysis …………………………………………………………………………………………

Blood count (Red and White) ……………………………………………………………………

Syphilis Test ……………………………………………………………………………………

T. B Test ………………………………………………………………………………………………

EyeTest ……………………………………………………………………………………

Additional information eg. Physical defect or impairment(s),chronic infections or family diseases…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above pupil and recommend that he/she is fit/ unfit to pursue further education

Signed ……………………………………………………………………………………………

Designation ………………………………………………………………………………………

Official Stamp:

Date: …………………………………

(Delete whichever is in applicable)

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule :0759868746**
- **Makamu Mkuu wa Shule :0767898247**